

Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir cha Wasilisha Kampeni

“MIAKA 25 BAADAYE: MAFUNZO KUTOKA SREBRENICA”

Mnamo 11 Julai, 1995, majeshi ya Serb yalivamia eneo la Waislamu la Srebrenica nchini Bosnia ambapo maelfu ya Waislamu walikuwa wametafuta himaya kutokana na mashambulizi ya jeshi la Serbia kaskazini mashariki mwa Bosnia. Mji huo ulikuwa umetengwa na Umoja wa Mataifa (UN) kama "eneo salama" na kutangazwa kuwa chini ya ulinzi wa UN. Siku zilizo fuatia kutekwa kwa Srebrenica, wanaume na wavulana wa Kiislamu 8000 waliuwawa kinyama na Waserbia hao. Ilitangazwa kuwa ndio ukatili mbaya zaidi kufanyika katika nchi ya Ulaya tangu Vita vya Pili vya Dunia. Sambamba na mauwaji haya, wanawake, watoto na wazee kati ya 25,000 na 30,000 walifurushwa kutoka mjini humo kama sehemu ya kampeni ya kikatili ya Kiserbia ya mauwaji ya kimbari ya Waislamu kutoka katika ardhi zinazo pakana na Jamhuri ya Serbia. Waislamu wa Srebrenica waliahidiwa ulinzi na Umoja wa Mataifa lakini ulinzi huo kamwe haukuja. Waliahidiwa kwamba serikali za kimagharibi zingesitisha mashambulizi ya Waserbia kupitia NATO lakini usaidizi huo kamwe haukuwa.



Mauwaji ya halaiki ya Srebrenica ni mojawapo tu ya msururu wa ukatili unaofanywa na majeshi ya Serbia dhidi ya Waislamu wa Bosnia katika vita vya Bosnia huku serikali za ulimwengu - za Waislamu na zisizokuwa za Waislamu - zikitazama. Vita vya Bosnia vya miaka mitatu, kuanzia 1992 hadi 1995, vilionyeshwa mauwaji ya kimbari ya Waislamu katika mamia ya miji na vijiji huku pande zote za Waserbia nchini Bosnia na serikali ya Jamhuri ya Serbia ya Slobodan Milosevic ikitafuta kuunda ruwaza yao ya kitaifa ya Serbia Tukufu, kwa eneo la Serbia lililo takata kutokana na ukabila kando kando ya Mto Drina. Watu 100,000 waliuwawa, 2.2 milioni kukosa makao na wanawake na wasichana wa Kiislamu 50,000 kunajisiwa na majeshi ya Serbia, huku wengi wakitungwa mimba kutokana na uhalifu huu wa kinyama. Maelfu ya Waislamu wa Bosnia pia waliwekwa kizuizini katika kambi za mateso ambapo walinyimwa chakula, kuteswa na kuuwawa.

Miaka kadhaa baada ya mauwaji ya halaiki ya Srebrenica, ulimwengu uliahidi, "Kamwe Haitatokea Tena" na kwamba mafunzo yatapatikana kutokana na doa hili jeusi katika historia ya sasa. Hata hivyo, leo tunaona chinja chinja na uhalifu wa vita vya Bosnia na mauwaji ya halaiki ya Srebrenica yakijirudia dhidi ya Waislamu kote ulimwenguni - ikiwemo nchini Syria, Myanmar, Kashmir, Palestina, Yemen, Turkestan Mashariki na India huku ulimwengu kwa mara nyengine tena unatazama. Mtume (SAW) amesema:

لَا يُلَدِّعُ الْمُؤْمِنُ مِنْ جُحْرِ وَاحِدٍ مَرَّتَيْنِ "Muumini hang'atwi katika tundu moja mara mbili." Hivyo, ni yapi mafunzo halisi yanayo paswa kusomwa kutokana na janga hili la kibinadamu? Vipi kumbukumbu ya matukio haya ya kinyama yaliyo pita yatatusaidia kuunda upya mustakbali wetu kama Waislamu ili kunali usalama na haki? Vipi tutaweza kuvunja turathi hii ya mauwaji ya halaiki yaliyo usibu Ummah wetu... ili historia isiendelee kujirudia?

Tunatarajia kuelezea kadhia hizi katika kapeni hii mpya.

Kampeni hii yaweza kufuatiliwa katika:

<http://www.hizb-ut-tahrir.info/en/index.php>

na <https://www.facebook.com/WomenSharia/>



WOMENANDSHARIA
WOMENFORKHILAFAT
WOMENSHARIAH3

#SREBRENICAMIKA25BAADAYE

